

MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA SIKU KUMI (01–10 JANUARY, 2018) NA MATARAJIO YA MVUA KWA SIKU KUMI (11 – 20 JANUARY, 2018)

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA SIKU KUMI (01–10 JANUARY, 2018)

Katika siku kumi za mwanzo za mwezi January 2018, migandamizo mikubwa ya hewa iliyo Kusini mwa Dunia (ST. Helena na Mascarene) iliendelea kudhoofika kidogo wakati ile iliyopo sehemu ya Kaskazini ya dunia (Azores na Siberia) iliendelea kuimarika kidogo na hivyo kuruhusu ukanda wa mvua (ITCZ) kuendelea kubaki Tanzania hususani katika meneo ya nyanda juu Kusini-Magharibi pamoja na maeneo ya kusini mwa nchi, hali hii ilipelekea kuwepo kwa vipindi vya mvua kubwa katika maeneo hayo. Joto la Bahari katika Bahari ya Hindi iliendelea kuwa juu kidogo ya Wastani ambalo lilisababisha maeneo ya Pwani kuwa na vipindi vya mvua. Kwa upande mwingine kumekuepo na joto la bahari la chini ya wastani katika eneo la Kusini-mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) hali iliyosababisha kuwepo vipindi vya mvua zinazoambatana na radi katika ukanda wa Ukanda wa Ziwa Viktoria na Magharibi mwa nchi

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA SIKU KUMI (01–10 JANUARY, 2018)

Mwenendo wa viashiria vya hali ya hewa hapo juu ulipelekea vipindi vya mvua zilizoambatana na radi katika maeneo ya nyanda za juu Kusini-Magharibi, mkoa wa Ruvuma, Ukanda wa Ziwa Viktoria, Magharibi na ukanda wa Pwani ya Kusini. Hata hivyo mikoa ya nyanda za juu Kaskazini-Mashariki, Pwani ya Kaskazini na yale ya Kati, iliweza kupata vipindi vichache vya mvua.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KATIKA SIKU KUMI (11 – 20 JANUARI, 2018)

2.1 VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA SIKU KUMI (11 – 20 JANUARI, 2018)

Katika kipindi cha siku kumi za pili za mwezi Januari, migandamizo mikubwa iliyopo Kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kudhoofika kidogo wakati migandamizo mikubwa iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuimarika kidogo. Ukanda wa mvua (ITCZ) utaendelea kubaki Tanzania hususani katika meneo ya nyanda juu Kusini-Magharibi pamoja na maeneo ya kusini mwa nchi, hali hii itapelekea kuwepo kwa vipindi vya mvua kubwa katika maeneo hayo. Joto la bahari la wastani linatarajiwa katika eneo la Kusini-magharibi mwa Bahari ya Hindi na hii inatarajiwa kusababisha kupunguza kwa mvua hususani ukanda wa Pwani ya Kaskazini. Kusini-mashariki mwa Bahari ya Atlantiki kunatarajiwa kuwepo kwa joto la juu ya wastani na hivyo kuchangia kupunguza kwa vipindi vya mvua katika ukanda wa Ukanda wa Ziwa Viktoria na Magharibi mwa nchi.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA SIKU KUMI (11–20 JANUARI, 2018)

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): Vipindi vya mvua vitakavyo ambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja navisiwa vya Unguja na Pemba): Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Vipindi vya mvua vitakavyo ambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Njombe, Iringa na Mbeya): Vipindi vya mvua vitakavyo ambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Vipindi vya mvua vitakavyo ambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma): Vipindi vya mvua vitakavyo ambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

Imetolewana; **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**